

## Bibilia ina maana gani inapozungumzia juu ya neema?

Kimsingi, ni fadhira za Mungu kwa wanadamu, na ni kweli kusema ‘fadhira tusizostahili, kwa maana hatujazifanya kazi kwa njia yoyote ile. Neno hili linaeleweka kwa upana zaidi kuwa ni neema ya Mungu inayotolewa kwa wale watu wanao weka matumaini yao kwa Yesu kwamba ni Bwana na Mwokozi. Muonekano halisi wa hiyo neema ni katika wokovu kwa wale wenye imani ya kweli. Hii haisemi ya kwamba chini ya sheria Mungu anadai haki kwa watu wote na ya kwamba katika neema Mungu anawapa neema wale waaminio. Ni kwa neema ya Mungu kwamba tunaokolewa, na si kwa haki yetu wenyewe. Ni kwa neema, na kwa neema tu kwamba tunaokolewa. ( Tazama Waefeso 2:1-9)

## Nyakati za neema zilianza duniani kupitia kifo na ufufuo wa Kristo Yesu

Tito 3:4-5; Yohana 1:17; 1:12-13, 3:36; Warumi 3:24-27; 5:2; 15-21; 6:14; 2 Wakorintho 6:1-3; 8:9; Wagalatia 1:3-15; 2:21; 5:4

Sheria (Kiebrania/ Torah) inaleta madai ya haki ya Mungu. Amri kumi (tazama Kutoka 20), na ufupisho wa sheria uliotolewa na Bwana wetu (Mathayo 22:37-40) ni mambo yenye umuhimu wa kipekee.

## Neema ni zawadi ya Mungu kumuwezesha mwanadamu kuishi maisha ya utakatifu

Kwahiyo inaweza kusemwa kwamba: sheria inadai – neema inatoa.

Kumbukumbu la Torati 5:6-22; 1 Yohana 4:19–5:21 (inaongelea juu ya upendo wa Mungu katika kumtoa Yesu, Mwana Wake); Yohana 1:12, 3:16; Warumi 3:21-24, 8:3, 10:4-10; Wafilipi 3:9, 4:13; Waebrania 7:19; Zaburi 51:11-17; Waefeso 5:15-20.

## Katika maisha tunaweza kuishi chini ya sheria, au chini ya neema

Huu ndiyo uchaguzi wa msingi unaomkabili kila mtu, iwapo wanaukubali au hawaukubali. Kumbukumbu za bibilia zinaonyesha wazi ya kwamba, chini ya sheria , kabla ya nyakati za Kristo, mwanadamu kwa ujumla alishindwa, na hatima yake alikuja kumsulubisha Yesu. Vilevile, hatima ya nyakati za neema itakuwa ni katika kushindwa kwa mwanadamu – na safari hii ushahidi mkubwa utakuwa ni katika mate-so dhidi ya Wayahudi, Wayahudi waaminio na Wakristo. Huu utakuwa ni wakati wa kuukataa ukweli – yamkini hata baadhi ya wale walio katika kanisa. Lakini anayeshindwa ni mwanadamu – si mpango wa Mungu wa neema.

2 Wakorintho 4:3–4; 2 Timotheo 3:1-8; 1 Yohana 4:1-3; 2 Petro 2:1; Yuda 4, 8, 11-13, 16.

## Urahisi na uhuru wa neema ni mpango wa Mungu wa wokovu wa ulimwengu

‘Injili’ nyingine yoyote si ya Mungu. Matendo 4:12; Warumi 10:9-13 (tazama Ezekieli 34); Wagalatia 1:8-9; Yohana 10:1-21

## Neema ya kawaida

Kuna mtazamo wa pili juu ya neema – wazo la neema ya kawaida. Kwa kuliweka kiurahisi, neema ya kawaida ni hali ya upendeleo wa Mungu kuititia upendo wake kwa mwanadamu unaodhihirishwa kwa njia ya Baraka zote anazozitoa pasipo wokovu. Kifungu cha muhimu kinachoonyesha jambo hili ni Matayo 5: 44-5.. 'Wapendeni adui zenu waombeeni wanaowaudhi, ili mpate kuwa wana wa Baba yenu aliye mbinguni, maana ye ye huwaangazia jua lake waovu na wema; huwanyeshea mvua weny haki na wasio haki...'

Mambo mengi ya maisha yanaweza kufurahiwa na kupatikana hata na wale wasio amini. Afya, urafiki, mafanikio na upendo wa kibinadamu yote yanapatikana kwa kila mtu wengine kwa wingi wengine kwa kiasi. Ukweli wa kwamba watu wengi wanashindwa kufurahia mambo haya ni kwamba kwa sehemu ni kwasababu ya ulimwengu tunaoishi ulio na dhambi na ulioanguka. Vifungu vinavyoonyesha wazo hili la neema ya kawaida ni: Zaburi 36:5-7; Zaburi 145:9, 14-17; Matendo 14:15-17; Matendo 17:24-28. Vifungu hivi vinashuhudia juu ya nia ya Mungu kwa watu wote. Tunapotenda dhambi na kuteseka kwaajili ya dhambi zetu, hii ni licha ya wema wa Mungu, na pia licha ya kipawa cha neema kuititia kwa Yesu. Hata hivyo, tunasisitizia kwamba njia kuu ya kuilewa neema inahusiana na kile Yesu alichokifanya msalabani.

Copyright © Sovereign World Trust, PO Box 777, TONBRIDGE, Kent, TN11 0ZS, UK  
[www.sovereignworldtrust.org.uk](http://www.sovereignworldtrust.org.uk)

### Publishing and Translation History

First Published in English by Glory to Glory Publications.

Christian Publications International, PO Box 212, Saffron Walden, CB10 2UU - [www.christian-publications-int.com](http://www.christian-publications-int.com)  
Editor Peter Sammons. Contributors Alex Jacob, David M. Moore, Peter Byron-Davies, Greg Stevenson, Peter Sammons  
ISBN English 978-0-9567831-6-5

This Kiswahili translation for Sovereign World Trust by Revd John Y Madinda with permission  
Swahili Edition Published by Sovereign World Trust ISBN - Kiswahili 978-1-908010-12-4